



CHUO KIKUU CHA NAIROBI

CHUO CHA SAYANSI ZA TIBA

HATI YA UTOAJI HUDUMA KWA UMMA

HUDUMA	MAHITAJI	GHARAMA	MUDA
Kutolewa kwa Barua za mwaliko kujiunga na Chuo Kikuu	Kutimiza Masharti ya Kujiunga na Chuo Kikuu	Hakuna malipo	Wiki nane (8) kabla ya tarehe ya kufika chuoni
Uelekezi wa Wanafunzi juu ya mazingira na taratibu za chuo	Kutimiza masharti ya kujiunga na Chuo Kikuu kwa Wanafunzi wa mwaka wa kwanza	Hakuna malipo	Wiki ya kwanza (1) baada ya kufika chuoni
Kutolewa kwa maelekezo ya mipango ya masomo, taratibu na kanuni za nidhamu kwa wanafunzi	Baada ya kujiunga na chuo na kusajiliwa	Hakuna malipo	Baada ya kusajiliwa
Kutolewa kwa Mihadhara na shughuli nyingine za mafunzo	Baada ya kulipa karo na ada nyinginezo zilizoidhinishwa	Kama ilivyolezwa katika barua ya mwaliko kujiunga na chuo	Kwa wakati ufaao na kwa mujibu wa ratiba zilizoidhinishwa
Usimamizi wa Miradi, Tafiti na Tasnifu za Uzamili na Uzamifu	Kumaliza na kupeleka karatasi na tasnifu za Uzamili na Uzamifu kwa wasimamizi	Hakuna malipo	Wanafunzi kupata maoni na majibu ya kazi zao wiki mbili (2) baada ya kuwasilisha kazi hizo
Orodha jumuishi ya alama za mitihani	Mitihani kusahihishwa na kuhitimishwa kwa wakati ufaao	Hakuna malipo	Wiki (4) baada ya mitihani kumalizika
Kesi za Nidhamu kwa Wanafunzi na Wafanyikazi	Kutayarishwa kwa mashtaka na tuhuma	Hakuna malipo	Kuhitimishwa katika kipindi cha siku thelethini (30) za utendakazi
Maktaba ya Tiba	Kadi ya utambulisho wa mwanafunzi/Kitambulisho cha mwanafunzi	Hakuna malipo	Kufunguliwa saa mbili asubuhi (8.00) hadi saa nne (10.00) usiku siku za wiki na saa mbili asubuhi (8.00) hadi saa kumi na moja (5.00) siku za Jumamosi na kuanzia saa nne

			asubuhi (10.00) hadi saa kumi (4.00) alasi siku za Jumapili
Sherehe za mahafali	Baada ya kumaliza na kuhitimu katika masomo ya chuo	Ksh. 3000/=	Kuandaliwa katika mwezi Disemba katika tarehe itakayotangazwa na Chuo Kikuu kila mwaka
Kutolewa kwa Vyeti na Nakala za Matokeo ya mitihani	Baada ya Mwanafunzi kupata vibali vya kuondoka kutoka shule na idara zote husika za chuo	Hakuna malipo	<ul style="list-style-type: none"> • Vyeti vya waliofuzu vitatolewa katika kipindi cha wiki (8) baada ya mahafali • Nakala za Matokeo ya mitihani zitatolewa katika kipindi cha wiki moja (1) baada ya kupokelewa kwa maombi
Kuajiriwa na Kupandishwa vyeo kwa Wafanyikazi	Kutimiza masharti ya Chuo Kikuu juu ya mahitaji ya Uajiri na Upandishwaji vyeo	Hakuna malipo	Kuhitimishwa katika kipindi cha wiki kumi na mbili tokea kutangazwa kwa nafasi hadi kutolewa kwa barua Uajiri au Upandishwaji vyeo
Tathimini za Utendakazi wa Wafanyikazi	Kujaza form za tathimini baada ya kuhudumu katika daraja fulani angalau kwa miezi sita katika mwaka kunapofanywa tathimini	Hakuna malipo	Kufanywa kati ya mwezi wa Oktoba na Machi kila mwaka
Ununuzi wa Bidhaa na Huduma	Kupata idhini zinazotakikana, kuwasilisha bidhaa na huduma zinazowiana na thamani kamili ya pesa zinazolipwa	Hakuna malipo	Kuhitimishwa katika kipindi cha wiki nane (8)
Uhasibu wa Fedha	Kuzingatia kanuni na taratibu za uhasibu za Chuo Kikuu	Hakuna malipo	Kushughulikia malipo yaliyoidhinishwa kwa muda usiozidi siku tatu (3)
Kupokelewa kwa simu kwa haraka	Mawasiliano yote yatapokelewa na kushughulikiwa kwa haraka	Hakuna malipo	Simu kujibiwa katika muda usiozidi sekunde ishirini (20)
Cheti cha Kibali cha Kuondoka Chuoni kwa Wanafunzi	Wanafunzi wataidhinishwa kupata Cheti cha Kibali cha kuondoka kutoka shule na idara zote husika	Madeni yote yanayowiwa Chuo kwa mujibu wa gharama zilizoonyeshwa	Kuhitimishwa kwa muda wa siku mbili (2)

UPOKEAJI MAONI NA MAJIBU

Malalamiko, pongezi na mapendekezo yatahitaji kuepeleka kwa wakuu wa idara husika, maelezo ya anwani zao yanapatikana katika tovuti ya Chuo Kikuu www.chs.uonbi.ac.ke

Rufaa zote kuhusiana na maoni au majibu ziwasilishwe kwa;

Mkuu wa Chuo
Chuo cha Sayansi za Tiba
Chuo Kikuu cha Nairobi
S.L.P. 19676—00200
NAIROBI

Simu: +254-020-2726300
Kipepesi (Fax): +254-020-2726300
Barua-pepe: principal-chs@uonbi.ac.ke
Tovuti: www.chs.uonbi.ac.ke